**Zawadi ya Mchanuliamaisha**

Abdul Adan
Extract translated by Richard Mabala

Siku mbili zilizopita nilifukuzwa kazi huko TSA (Transportation Security Administration - Idara ya Usalama wa Usafiri) kwenye uwanja wa ndege. Bosi wangu alimshawishi mjinga fulani aliyechukizwa na mimi kunifungulia mashtaka kwamba nimemnyanyasa kijinsia. Hii ilikuwa kama jambo la kipuuzi kabisa. Kila mtu kazini anajua kwamba mimi si shoga. Sina hisia za kuwataka wanaume kimapenzi. Hii najua mwenyewe, wafanyakazi wenzangu wanajua na bosi wangu anajua. Hata yule mjinga aliyechukizwa anajua. Mimi si mtu wa kumpenda mwanamume mwingine kimapenzi. Mara kabla ya kunipatia habari hii ya kusononesha, bosi wangu mshenzi asiye na upendo (Yaani, ungemwona huyu mpumbavu! Ana pua ya mifupa isiyopendeka) alijikalifu kunifafanulia hatia ninayotuhumiwa. Alisema kwamba nina mwelekeo wa *kutua* wakati nawasachi watu.

Sikatai, nimewahi kutumia neno *kutua*. Lakini halikuwa jambo la kutisha kama bosi alivyosingizia. Ilikuwa ni mzaha tu wa chumba cha mapumziko. Mfanyakazi mwenzetu wa kike kutoka mitaa ya katikati ya mji alikuwa amemwaga kahawa na kuinama kuifuta. Alikuwa amevua sare yake ya TSA na kuiweka kwenye kasha. Nadhani alikuwa amemaliza shifti yake. Basi, kwa jicho la wizi, nilipata kuona maziwa ya yule mama yalivyoning'inia, ghafla akajitokeza yeye. Akilini mwangu, nilimwona Ted Lifebloom mwenyewe alikuwa amepiga magoti kulia kwake akijaribu kuingiza mikono yake minene humu. Lakini Ted hakuwa tena mtoto mwenye kumpenda mama yake. Alikuwa bonge la mtu mzima na mikono yake ilishindwa kupita kwenye nafasi ndogo kati ya kwapa na fulana. Kwa hiyo alilala chini yake, mikono juu, akamvuta hadi akapiga magoti na kutamka kwa sauti kwamba alitaka *kutua* pale daima dumu. Sasa *mimi* sikufanya hayo hata kidogo, sikutafuta kale kanafasi, wala siku*tua* kati ya kiwiliwili chake kilichoinama na sakafu. Bila kuleta madhara yoyote, nilimwambia msimamizi wangu ambaye alikuwa rafiki kwamba mtu angeweza *kutua* kati yake yeye na sakafu. Unaona, ilikuwa neno ambao mtu asingeweza kujizuia, kulingana na hali ile. Kwa mintarafu ya 'mwelekeo' ambao bosi wangu ananishtaki, nilitumia neno hili mara moja tu zaidi. Haitoshi kuitwa 'mwelekeo'.

Mara mojamoja, msafiri hujitokeza anayeonekana kuwa Ted Lifebloom. Haidhuru awe mwanamume au mwanamke kwa sababu tunu mahsusi la Ted Lifebloom si tunu linaloendana na jinsi fulani. Wako wanaume na wanawake wengi duniani wenye nyuso nenenene, vifua laini (viwe bapa, viwe vimejaa haidhuru) na shingo za mviringo na vile vizingo vinene vya kuamsha ashiki. Inaweza kuonekana rahisi nikielezea hivyo lakini, hebu nisikilize hadi mwisho. Tunu mahsusi haitokani na sifa zile zilizotajwa hapo juu, zaidi ni kama sifa hizi zinamfanya mtu astahili tunu hili. Inabidi mtu aguswe na Ted au kuwa mwanafunzi wa Ted ili kuelewa tunu. Watu wengi sana hawana habari kuhusu nafasi yao mahsusi ulimwenguni. Maelfu au hata mamilioni ya Lifebloomers.

Asubuhi ile, mwanamume Mturuki alipita kwenye mlango wa ukaguzi kwenye Uwanja wa Ndege wa Lambert. Nilitambua mara tu aliponisogelea ili asachiwe kwamba alikuwa Lifebloomer. Nilijuaje? Basi tuseme tu kwamba alikuwa na uso nenenene na kitone cha jasho ndeweni mwake. Kwa kuwa mimi ni mkarimu sana, niliamua papohapo kumtafakarisha, kwa namna erevu sana, uTed moyoni mwake. Mara nyingi upande wa Lifebloomers wenye nyuso nenenene (tofauti na wale wenye mikono iliyojaa nywele na mafungo ya unene chini ya tumbo lao) wanakuwa na baka jeusi nyuma ya magoti yao. Ili kuwatafakarisha inabidi kutambua baka hili na dole gumba la kulia na kuligandamiza. Kwa bahati nzuri, msafiri huyu alikuwa amevaa kaptula, jambo ambalo lilirahisisha kazi. Nilihitajika kumpapasa mwili mzima na kutulia nyuma ya goti lake. Kisha ninge*tua* mara moja kwenye baka. Msinielewe vibaya; natambua kwamba hii inaonekana la kutisha/tia kinyaa kwa wale wasioelewa. Lakini nilitumia akili. Mara nilipofikia baka jeusi, nilipata changamoto wa kufikiria mbinu ya kuvuta muda. Nilihitaji

kisingizio kizuri cha kuweza kugandamiza kidole gumba changu palepale nyuma ya goti kwa nukta thelathini.  Bila shaka utaelewa kwamba hii si kazi rahisi. Basi nilifanya hivi:

Nilipitisha mikono yangu kwenye mwili wake kuanzia kwa mabega, nikitua kulingana na utaratibu kwenye mifuko, na nilipofika kwenye eneo ambalo niliona baka litakuwepo, nilijifanya nina kizunguzungu.  Nikiegemea mkono wangu wa kushoto uliokuwa umejikita sakafuni, nilijisikia nimejaa furaha uso na kifani, nikiwa nimesisimka kutokana na kitu cha Lifeblooming kilichojificha kwenye baka. Sawa na Lifebloomers wote wajinga, yule mwanamume akatingisha mguu kwa nguvu ili kuondoa mkono wangu lakini nilifanikiwa kuendelea kushika kwa nukta 30 kamili.  Alipolalamika baadaye ilikuwa bure.  Kila mtu alijua kwamba nina pua inayoathirika kirahisi sana.  Kwa vyovyote, viatu vyake vilivyonuka, kama ambavyo mtu yeyote kwenye akili angedhani, vilisababisha kizunguzungu changu papohapo.  Hata hivyo, nilimwambia bosi wangu asiye na akili (ambaye alihifadhi taarifa ya tukio) kwamba marashi ya msafiri yalinipa kichefuchefu na kidogo nizimie kabisa kwa nukta kadhaa - nilihitaji kuegemea goti lile.  Sidhani kama aliniamini hapo lakini ukweli ni kwamba nani anajali?  Huwezi kumwachisha mtu kazi kwa sababu pua yake huathirika mno, sembuse kwa kuwa Lifebloomer. (Mchanuliamaisha)